*Jina la Mwanafunzi*_____ *Shule*_____

*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*_____ *Tarehe ya Upimaji*_____

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
UMOJA WA SHULE ZA MISHENI

ORGANIZATION

0595

UPIMAJI WA PAMOJA AWAMU YA KWANZA, DARASA LA NNE - 2026

A07 **SOMO: HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

MUDA: Saa 1.30 **Ijumaa, Machi 27, 2026**

Maelekezo:

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, na C zenye jumla ya maswali sita (6)
2. Jibu maswali yote **kwa usahihi** katika kila sehemu kwa kutumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**
3. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani
4. Andika **jina lako, namba ya upimaji, na jina la shule yako sehemu ya juu** katika kila ukurasa

SEHEMU A (Alama 20): Jibu maswali yote katika sehemu hii
1. Chagua herufi ya jibu sahihi na ujaze katika kisanduku ulichopewa

(i) Ni kiashiria kipi kilimwezesha binadamu aliye msituni peke yake kutambua kuwa anakaribia mji? [ ]
(a) Jua kali (b) Sauti za watu (c) Moshi (d) Paa la nyumba

(ii) Kama mtoto ana haki ya kulindwa; ni wajibu gani alio nao mtoto kwa kuzingatia haki hiyo ya kulindwa?
(a) Kucheza (b) Kudhurula (c) Kufurahi (d) Kujilinda na kulinda wengine [ ]

(iii) Nini umuhimu wa kusalimiana kama kitendo cha maadili katika jamii? [ ]
(a) Kufungua ukurasa mpya wa mahusiano mema (b) Kuanzisha usengenyaji
(c) Kutoa taarifa (d) Kueneza chuki

(iv) Ni njia gani ilitumika katika jamii za kale kuwafundisha watoto na vijana maadili? [ ]
(a) Masimulizi ya hadithi (b) Kusoma vitabu
(c) Mafunzo kwenye mapango (d) Majaribio ya kuua wanyama wakali

CamScanner

*Jina la Mwanafunzi*_____ *Shule*_____
*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*_____ *Tarehe ya Upimaji*_____

(v) Baba yake wa mama anaitwaje? [ ]
(a) Baba mkubwa (b) Baba wa mama (c) Bibi (d) Babu

(vi) Ni tabia ipi kati ya tabia zifuatazo sio nzuri kwa usitawi wa mtu binafsi na jamii yake?
(a) Ushindani (b) Kujaliana (c) Kuheshimiana (d) Kusaidiana [ ]

(vii) Binadamu alianza kutengeneza zana kama vile mikuki na visu katika zama gani za mawe?
(a) Zama za mawe za kati (b) Zama za mawe za mwisho [ ]
(c)Zama za mawe za kale (d) Zama za mawe za mwanzo

(viii) Ni ipi faida ya ujio wa wageni kutoka Mashariki ya Mbali na Kati? [ ]
(a) Kutumikishwa kazi ngumu (b) Biashara ya watumwa
(c) Ukuzaji wa misamiati ya lugha ya Kiswahili (d) Kuanzishwa magereza

(ix) Ni upi umuhimu wa kiuchumi wa urithi wa Sanaa za kale katika taifa letu? [ ]
(a) Kuchochea maendeleo ya kiuchumi kupitia utalii
(b) Kutoa ushaidi wa chimbuko la tamaduni zetu
(c) Kutambulisha urithi uliopo nchini
(d) Kupata historia ya jamii zetu

(x) Kaka yangu Mwasha amesomea taaluma ya uchunguzi wa kisayansi kuhusu masalia ya mambo ya kale na utamaduni wa binadamu; taaluma hii inaitwaje? [ ]
(a) Historia (b) Anthropolojia (c) Akiolojia (d) Jiolojia

2. Oanisha maana au jukumu katika sehemu A na msamiati au kundi husika katika sehemu B

Sehemu A	**Jibu**	**Sehemu B**
(i) Sanaa inayoeleza historia ya kale ya Kitanzania	[ ]	A. Wazee
(ii) Kupambana na maadui wa jamii yao	[ ]	B. Jando
(iii) Kuwafundisha vijana kazi na maadili	[ ]	C. Vijana
(iv) Mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wasichana kuhusu maisha, mila , na desturi	[ ]	D. Unyago
(v) Mafunzo ya nadharia na vitendo kwa wavulana kuhusu maisha, mila , na desturi	[ ]	E. Ususi
		F. Uchoraji

CamScanner

*Jina la Mwanafunzi*_____ *Shule*_____
*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*_____ *Tarehe ya Upimaji*_____

3. Jibu kipengele (i)-(v) kwa kuchagua jibu sahihi kwenye jedwali kisha uandika jibu kwa usahihi sehemu iliyoachwa wazi

Mbale,	Kitali,	Shaba,	Chumvi,	Dhahabu,	Chuma,	Tanzanite

i. Udongo wenye chembe chembe za madini ya chuma huitwa? .....

ii. Madini maarufu Katanga .....

iii. Madini maarufu Mereranei, Arusha, Tanzania.....

iv. Madini maarufu Uvinza, mkoani Kigoma .....

v. Malighafi ya chuma iliyotumika kutengenezea zana mbalimbali za chuma .....

.....

Sehemu B (Alama 18): Jibu maswali yote katika sehemu hii

4. Chunguza kielelezo kifuatacho kwa makini kisha jibu vipengele (i)-(v) vifuatavyo:



Kielelezo 1

(i) Ni shughuli gani inaonyeshwa katika picha hii?.....

(ii) Mtu anayefanya shughuli iliyoonyeshwa katika **Kielelezo 1** anajulikana kama.....

.....

(iii) Taja zana mbili zilizopatikana kutokana na shughuli iliyoonyeshwa katika **Kielelezo 1** hapo juu. a. ..... b. .....

(iv) Taja shughuli mbili zilizofanywa na zana zilizozalishwa kutokana na shughuli iliyoonyeshwa katika **Kielelezo 1** hapo juu.

a..... b.....

(v) Ni madini gani yanatumiwa kama malighafi katika shughuli iliyoonyeshwa katika **Kielelezo 1** hapo juu? .....

CamScanner

*Jina la Mwanafunzi*_____ *Shule*_____
*Namba ya Upimaji ya Mwanafunzi*_____ *Tarehe ya Upimaji*_____

5. Andika majibu mafupi ili kujibu vipengele (i)-(iv) katika swali hili:

(i) Mkusanyiko wa sheria na kanuni zinazoainisha jinsi nchi itakavyoendeshwa huitwa.....
.....

(ii) ..... ni miti midogo mirefu mfano wa fimbo, zilizosukwa kwa kamba kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za asili.

(iii) Maeneo yenye kuhifadhi vitu vyenye urithi wa kiasili na utamaduni huitwa.....

(iv) 'Kidole kimoja hakivunji chawa'. Wazee hutumia methali hii kuhimiza.....
.....kwa vijana wao.

Sehemu C (Alama 12): Jibu swali la sita (6)

6. Soma kifungu cha habari kisha jibu maswali yafuatayo:

Wakoloni walioitawala Tanganyika ni Wajerumani na Waingereza. Wakoloni wa kwanza kuitawala Tanganyika walikuwa Wajerumani baadae wakifuatia Waingereza. Baadae Tanganyika ilipata uhuru wake mnamo tarehe 9/12/1961. Waziri mkuu wa kwanza wa Tanganyika aliitwa Julius Kambarage Nyerere na baadaye akawa rais wa kwanza wa Tanganyika mnamo terehe 9/12/1962.

Maswali:

(i) Wakoloni wa kwanza kuitawala Tanganyika walikuwa ni .....

(ii) Waziri mkuu wa kwanza wa Tanganyika aliitwa .....
.....

(iii) Tanganyika ilipata uhuru wake mwaka .....

(iv) Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa Rais wa Tanganyika mwaka .....
.....

(v) Taja aina mbili za wakoloni walioivamia na kuitawala Tanganyika
(a) .....
(b) .....

(vi) Rais wa kwanza wa Tanganyika huru aliitwa nani? .....
.....

CamScanner